

### MUHTASARI

- Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinataraajiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Ruvuma, Lindi na Mtwara. Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani zinataraajiwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Njombe, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro.
- Katika nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2022 – Januari, 2023) vipindi virefu vya ukavu vinataraajiwa kujitokeza.
- Ongezeko la mvua linataraajiwa katika nusu ya pili ya msimu (Februari- Aprili, 2023). Aidha, mvua za nje ya msimu zinataraajiwa mwezi Mei, 2023 katika maeneo mengi.
- Maeneo ya mikoa ya Singida na Dodoma mvua za **Msimu** zinataraajiwa kuanza kwa kuchelewa katika wiki ya pili ya mwezi Januari, 2023.
- Katika kipindi cha Novemba na Disemba, 2022, upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika udongo unataraajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayopata mvua za Msimu na kuathiri ukuaji wa mazao na upatikanaji wa malisho kwa ajili ya mifugo.

### MWELEKEO WA MIFUMO YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA NOVEMBA, 2022 HADI APRILI, 2023

Hali ya sasa ya joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la kati la Bahari ya Pasifiki inataraajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani (La Niña) katika nusu ya kwanza ya msimu ingawa joto linataraajiwa kuongezeka kidogo hasa katika nusu ya pili ya msimu. Vilevile, joto la bahari linataraajiwa kuwa chini ya wastani katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi na juu ya wastani mashariki mwa Bahari ya Hindi joto hususan katika nusu ya kwanza ya msimu. Kwa ujumla hali hii inataraajiwa kupunguza upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea nchini na hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua hasa katika maeneo ya kanda ya pwani ya kusini, kusini na mikoa ya kanda ya kati ukilinganisha na eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki). Hali hii inataraajiwa kupunguza nguvu ya mifumo inayosababisha mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kusini na yale ya kati mwa nchi. Vilevile, joto la bahari la chini ya wastani linataraajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu, na juu kidogo ya wastani katika nusu ya pili ya msimu. Hali hiyo inataraajiwa kupunguza uwezekano wa kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kuchelewesha mifumo inayosababisha mvua katika

maeneo ya kusini mwa nchi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu. Hali kadhalika, joto la bahari la chini kidogo ya wastani katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (nje ya pwani ya Angola) sambamba na joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi linataraajiwa kupelekea msukumo hafifu wa upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi yetu ikijumuisha maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi.

### MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU NOVEMBA, 2022 HADI APRILI, 2023

Mvua za **Msimu** (Novemba, 2022 – Aprili, 2023) ni mahusus kwa maeneo ya magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo yaliyopo kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa, mvua za chini ya wastani hadi wastani zinataraajiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Ruvuma, Lindi na Mtwara. Aidha, mvua za wastani hadi chini ya wastani

### **Na. 28 Toleo Maalum:**

zinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Njombe, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro. Mvua zinatarajiwa kuanza kwa kuchelewa na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu hususan katika nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2022 – Januari, 2023). Hata hivyo, ongezeko la mvua linatarajiwa katika nusu ya pili ya msimu (Februari - Aprili, 2023). Aidha, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa mwezi Mei, 2023 katika maeneo mengi.

Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

#### **Kanda ya magharibi (Tabora, Katavi na Kigoma):**

Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2022 katika maeneo mengi na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2023. Aidha, kuna uwezekano wa mvua za nje ya msimu mwezi Mei, 2023.

#### **Kanda ya kati (Singida na Dodoma):**

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani na zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Januari na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2023. Aidha, kuna uwezekano wa mvua za nje ya msimu mwezi Mei, 2023.


#### **Nyanda za juu kusini magharibi (Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo haya. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Disemba, 2022 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2023. Aidha, kuna uwezekano wa mvua za nje ya msimu mwezi Mei, 2023.

#### **Pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa nchi: (Lindi, Mtwara na Ruvuma):**

Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo haya. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Disemba, 2022 katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ikiambatana na vipindi virefu vya ukavu katika mwezi Disemba, 2022 na Januari, 2023 katika mkoa wa Ruvuma. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2023. Aidha, kuna uwezekano wa mvua za nje ya msimu mwezi Mei, 2023.

### **Msimu wa mvua za Msimu Novemba, 2022 hadi Aprili, 2023**



**Kielelezo 1: Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2022 –Aprili, 2023)**

## **ATHARI NA USHAURI**

### **Sekta ya kilimo na usalama wa chakula**

Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi yanayopata mvua za **Msimu** zinaweza kusababisha upungufu wa unyevunyevu katika udongo. Hali hii inaweza kuathiri uoteshaji na ukuaji wa mazao hususan katika kipindi cha Novemba na Disemba, 2022. Aidha, ongezeko la visumbufu vya mazao kama vile mchwa, viwavijeshi, panya vinatarajiwa kujitokeza katika msimu na hivyo kuathiri mazao na uzalishaji kwa ujumla. Matukio ya moto yanaweza kujitokeza kutokana na vipindi virefu vya ukavu vinavyotarajiwa.

Wakulima wanashauriwa kupanda mazao na mbegu zinazokomaa kwa muda mfupi na zinazostahimili upungufu wa mvua kama vile mazao jamii ya mizizi, mikunde na mazao ya bustani. Aidha, inashauriwa kutumia mbinu na teknolojia bora za kilimo himilivu za kuhifadhi maji na unyevunyevu wa udongo ikiwa ni pamoja na uvunaji wa maji ya mvua na matumizi ya matandazo. Wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuzingatia ushauri na tabiri zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo.

Mamlaka husika zinashauriwa kutoa elimu na ushauri kwa wakulima juu ya njia bora na namna ya kutumia kiwango kidogo cha mvua kinachotarajiwa, pamoja na matumizi mazuri ya akiba ya chakula kilichopo.

### **Mifugo na Uvuvi**

Upungufu wa mvua hususan katika nusu ya kwanza ya msimu unatarajiwa kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na kupelekea uwezekano wa migogoro kujitokeza baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, baadhi ya magonjwa ya mifugo (yanayoenezwa na kupe na wadudu warukao) pamoja na uzalishaji wa mifugo na mazao ya mifugo vinatarajiwa kupungua. Upatikanaji wa chakula kwa ajili ya samaki unatarajiwa kupungua na kuathiri mazao ya

samaki. Aidha, kilimo cha mwani kinachofanyika katika maji ya kina kifupi kinaweza kuathirika kutokana na vipindi virefu vya ukavu.

Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupanda malisho ya kutosha yanayoweza kustahimili ukame, kuweka mipango mizuri ya matumizi na uhifadhi wa maji na malisho, kufuga kibiashara (kupunguza idadi ya mifugo) na kuvuna mifugo kulingana na upatikanaji wa malisho na maji. Aidha, wadau wa sekta kwa ujumla, wanashauriwa watumie taarifa za utabiri wa hali ya hewa na kuzingatia ushauri wa maafisa ugani.

#### ***Utalii, Maliasili na Wanyamapori***

Upungufu wa mvua unaotarajiwa katika maeneo mengi unaweza kusababisha upungufu wa maji na malisho kwa wanyamapori na kupelekea wanyamapori kuhama kwa ajili ya kutafuta maji na malisho. Hali hii inaweza kusababisha migogoro kati ya wanyamapori na binadamu na kusambaa kwa magonjwa. Halikadhalika, uzalishaji wa asali unatarajiwa kuathirika kutokana na upungufu wa maji.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa. Hata hivyo, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika iwapo wanyamapori wataingia katika makazi au maeneo mbalimbali ya watu.

#### ***Mamlaka za maji na Menejimenti za Maafa***

Kutokana na matarajio ya upungufu wa mvua, Mamlaka za Miji zinashauriwa kutumia fursa hii katika kuendelea kufanya marekebisho ya miundombinu mbalimbali kama vile barabara, madaraja, majengo, sehemu za kuhifadhi taka, maghala, njia za umeme pamoja na kuhakikisha kuwa mifumo ya maji safi na maji taka inafanya kazi katika kiwango kinachostahili. Pia Mamlaka zinashauriwa kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa pamoja na kuweka miundombinu ya uvunaji maji ili kuzuia upotevu wa maji kwa matumizi endelevu ya baadae. Vilevile, Mamlaka za Miji zinashauriwa kuhamasisha na kukamilisha ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara, madarasa, hospitali na miundombinu mingine iliyopangwa katika kipindi hiki.

Upungufu wa mvua unaoweza kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi unaweza kusababisha upungufu wa unyevunyevu katika udongo, chakula, malisho ya mifugo na maji.

Aidha, uharibifu wa miundombinu, upotevu wa mali na madhara kwa binadamu vinaweza kutokea kutokana na vipindi vifupi vya mvua kubwa vinavyoweza kujitokeza. Hivyo, mamlaka husika na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Vijiji zinashauriwa kushirikiana na kuchukua hatua za kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na maafa ikiwemo kutoa elimu na miongozo itakayo hamasisha kilimo cha mazao yanayo stahimili ukame, uhifadhi wa chakula, maji na malisho ya mifugo.

#### ***Angalizo 1:***

***Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.***

#### ***Angalizo 2:***

***Upo uwezekano wa kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi ikiwa ni pamoja na rasi ya Msumbiji, hivyo kusababisha vipindi vya mvua katika nusu ya pili ya msimu.***

#### ***Angalizo 3:***

***Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi.***

***Watumiaji wa taarifa za utabiri huu Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.***